JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA BAGAMOYO

**Kumb. Na.** HWB/A.20/76/VOL.I/15 24/05/2022

# TANGAZO

# NAFASI ZA AJIRA KADA MBALIMBALI

Kwa mujibu wa kibali cha ajira mpya Kumb.Na. **FA.97/228/01/9** cha tarehe **13/05/2022** Kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo anapenda kuwatangazia Watanzania wote wenye sifa kuomba nafasi ya Ajira mbalimbali kwa masharti ya kudumu.

Mchanganuo wa kazi ni kama ifuatavyo :-

**1. Katibu Mahususi III – Nafasi 3**

**I: KAZI NA MAJUKUMU**

1. Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida.
2. Kusaidia kupokea wageni na kuwasikiliza shida zao na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa.
3. Kusaidia kutunza taarifa/Kumbukumbu za matukio, miadi, wageni, tarehe za Mikutano na vikao, safari za Mkuu wake na ratiba ya kazi zingine zilizopangwa kutekelezwa katika Ofisi unayofanyia kazi na kumualifu Mkuu wake na wakati unaohitajika.
4. Kusaidia kutafuta na kumpatia Mkuu wake majalada/nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi hapo Ofisini.
5. Kusaidia kufikisha maelekezo ya Mkuu wake wa kazi kwa wasaidizi wake na pia kumuarifu kuhusu taarifa zozote anazokuwa amepewa na wasaidizi wake.
6. Kusaidia kupokea majalada, kuyagawa kwa maofisa walio katika sehemu alipo, kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika.
7. Kutekeleza kazi zozote atakazokuwa amepangiwa na msimamizi wake wa kazi.

**II: SIFA ZA MWOMBAJI**

1. Awe amehitimu kidato cha nne IV na kuhudhuria mafunzo ya Uhazili (cheti NTA-LEVEL 5) na kufaulu mtihani wa hatua ya tatu kutoka Chuo cha Utumishi wa Umma au Vyuo vingine vinavyotambulika na Serikali.
2. Awe amefaulu somo la Hati mkato ya Kiswahili na Kiingereza maneno 80 kwa dakika moja.

*Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W)*
**Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya Bagamoyo, S.L.P. 59, BAGAMOYO Mkoa wa Pwani.**
**Simu Na: 023 2440164, Nukushi: 023 2440338 Barua Pepe: ded.bagamoyo@pwani.go.tz. Tovuti: www.bagamoyodc.go.tz**

3. Awe amepata mafunzo ya Kompyuta kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali na kupata Cheti katika program za Windows, Microsoft Office, Internet email and Publisher.

III: **MSHAHARA**
TGS BI kwa mwezi

**2. NAFASI YA KAZI: DEREVA DARAJA II (NAFASI 4)**

**KAZI NA MAJUKUMU**

1. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya Usalama wa Ajali
2. Kuwapeleka Watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.
3. Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari
4. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali.
5. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari (Log Book).
6. Kufanya Usafi wa gari na
7. Kufanya kazi nyingine kadri utakavyoelekezwa na msimamizi wake.

**SIFA ZA KUAJIRIWA**

Kuajiriwa mwenye elimu ya kidatu cha IV/VI na leseni ya daraja E au C1 ya uendeshaji magari ambayo ameyafanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila ya kusababisha ajali. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari(Basic Driving Course) yanayotolewa na chuo cha Mafunzo ya ufundi Stadi (VETA)au chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali Waombaji wenye vyeti vya majaribio ya Ufundi daraja II watafikiriwa kwanza.

**MSHAHARA**

TGS BI kila mwezi

**MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE AMBAYO NI LAZIMA KUZINGATIWA.**

1. Mwombaji lazima awe ni Raia wa Tanzania.
2. Awe hajawahi kufungwa kwa makosa ya jinai.
3. Awe hajawahi kupunguzwa/kufukuzwa kazi Serekalini.
4. Maombi ni lazima yaambatanishwe na vivuli vya vyeti vya kuzaliwa, kuhitimu elimu ya sekondari (Result Slip hazikubaliki) na vyuo vya mafunzo ya taaluma.
5. Maombi ni lazima yaambatanishwe na picha mbili za passport size za hivi karibuni.
6. Maombi ni lazima yaambatanishwe na wasifu(Curriculum Vitae) zenye mawasiliano ya uhakika, Anuani, Barua pepe na Namba ya Simu.
7. Awe na umri wa zaidi ya miaka 18 na usiozidi miaka 45.
8. Mwombaji awe hajawahi kuajiriwa Serekalini na kupata Cheki Namba.

9. Waombaji wenye vyeti vya kidato cha nne na vyeti vya taaluma ambavyo vimepatikana nje ya nchi wahakikishe vimehakikiwa na Baraza la Taifa la Mtihani (NECTA) na Baraza la Elimu ya Ufundi la Taifa (NACTE)

**MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI HAYA NI TAREHE 5/06/2022 SAA 9:30 ALASIRI PIA MAOMBI YOTE YATUMWE KWA NJIA YA POSTA KWA KUTUMIA ANUANI HAPO CHINI NA SI VINGINEVYO.**

**MKURUGENZI MTENDAJI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA BAGAMOYO**
**SLP 59,**
**BAGAMOYO.**

**TANGAZO HILI PIA LINAPATIKANA KWENYE TOVUTI YA HALMASHAURI www.Bagamoyodc.go.tz, Mbao za Matangazo, Ofisi za Kata, Tovuti ya Sekretarieti ya Ajira www.Sekretarieti. go.tz na Mitandao ya Kijamii.**

**TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA:**

Shauri Selenda
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**HALMASHAURI YA WILAYA**
**BAGAMOYO.**

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA
BAGAMOYO

**Nakala:** Katibu Mkuu,
Ofisi ya Rais,
Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma,
S.L.P 2320
**DODOMA**